**HOTUBA YA MGENI RASMI BALOZI MHANDISI JOHN W. H. KIJAZI, KATIBU MKUU KIONGOZI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA WAHANDISI NCHINI, KATIKA UKUMBI WA DKT. JAKAYA KIKWETE, DODOMA, TAREHE 3 SEPTEMBA, 2020**

***Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;***

***Arch. Elius A. Mwakalinga, Katibu Mkuu wa Sekta ya Ujenzi katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;***

***Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wote Mliopo;***

***Wakuu wa Wilaya mliohudhuria;***

***Mhandisi Prof. Ninatubu Lema, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi;***

***Wenyeviti wa Bodi mbalimbali mliopo;***

***Wajumbe wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi;***

***Mhandisi Patrick Barozi, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi;***

***Wageni kutoka Nchi za Nje ambao wanashiriki nasi kwa njia ya mtandao;***

***Wakuu wa Taasisi mbalimbali katika Sekta ya Ujenzi na Taaluma ya Uhandisi;***

***Wadau wa Sekta ya Ujenzi;***

***Wahandisi wote wa fani mbalimbali mliohudhuria mkutano huu;***

***Wageni wote Waalikwa;***

***Wanahabari wote mliohudhuria;***

***Mabibi na Mabwana.***

Habari za mchana!

1. Kwanza kabisa napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena leo katika

maadhimisho haya ya Siku ya Wahandisi kwa mwaka huu wa 2020. Nachukua fursa hii kuwashukuru wote kwa kuja kushiriki kwa wingi kwenye maadhimisho haya. Nawapongeza Wahandisi wote wa Tanzania kwa kufanya maadhimisho haya kwa mara ya 17 mfululizo tangu yalipoanzishwa mwaka 2003. Aidha, kwa wale wote waliotoka nje ya Mkoa wa Dodoma, napenda kuwakaribisha katika jiji letu hili la Dodoma, ambalo ndio Makao Makuu ya Nchi.

Vilevile, naipongeza Wizara husika pamoja na Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa kuandaa maadhimisho haya kwa mara nyingine kwa ufanisi mkubwa.

Kwa namna ya pekee, naishukuru Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kunialika kuja kuzungumza na Jumuiya hii ya Wahandisi na Washiriki wengine katika maadhimisho haya.

***Ndugu Wahandisi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

2. Nimejulishwa kuwa tunao wageni ambao wanashiriki nasi katika mkutano huu kwa njia ya mtandao kutoka Uganda, Botswana, Zimbabwe, Nigeria, Kenya, Rwanda na Balozi wa Norway hapa nchini Tanzania. Nawashukuru Wageni wetu hao kwa ushiriki wao, kwani hii inadhihirisha jinsi wanavyoshirikiana kwa karibu na Wahandisi wenzao wa hapa Tanzania kwa faida ya nchi zetu.

   Napenda kuwafahamisha Wageni wetu hao kuwa, baada ya janga la COVID-19 kwisha, tunawakaribisha sana kuja Tanzania kushiriki nasi katika mikutano kama hii ya miaka ijayo kwani tunapenda kuona ushirikiano huu baina ya Wahandisi wa nchi zetu ukiendelea kuimarika.

*Ndugu Mwenyekiti wa Bodi;*

3. Kama nilivyosema awali, napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Bodi ya Usajili ya Wahandisi, Menejimenti pamoja na Sekretarieti yote ya Bodi kwa kuandaa mkutano huu muhimu.

   Nimejulishwa kwamba Mkutano huu wa siku mbili unahudhuriwa na wahandisi wapatao **3,700** wa fani mbalimbali waliopo ndani ya ukumbi huu. Pia, nimejulishwa kuwa Wahandisi wengine wengi wanafuatilia mkutano huu kwa njia ya mtandao kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini na kutoka nje ya nchi pia. Vilevile, nimejulishwa kwamba washiriki wa mkutano huu mtajadili Mada Nane (8) muhimu katika sekta mbalimbali; zote zikilenga katika Mada Kuu ambayo ni ***"Mapinduzi ya Nne ya Viwanda ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu: Changamoto na Fursa kwa Wahandisi".*** Kwa lugha ya Kiingereza Mada hii tafsiri yake ni ***"4th Industrial Revolution Towards Achieving Sustainable Development Goals (SDGs): Challenges and Opportunities for Engineers."***

   Mada hii kuu mliyoichagua ni muafaka kwa wakati huu tuliopo kuliko wakati mwingine wowote. Wote tunafahamu jinsi Serikali ya Awamu ya Tano ilivyoamua kukuza uchumi wa viwanda katika nchi yetu. Hivyo, ni matumaini yangu kuwa mada hizo Nane mtakazojadili zitasaidia kutoa mwelekeo wa jinsi ya kutumia taaluma na ubunifu wenu wa kihandisi kwa kushirikiana na taaluma nyingine katika kuimarisha uchumi wetu wa Viwanda. Ni imani yangu kuwa kupitia mkutano huu mtaibua maeneo yote muhimu ya fursa zilizopo zinazohitaji kufanyiwa kazi na changamoto zilizopo zinazohitaji kutatuliwa ili kufanikisha mapinduzi ya Nne ya

Viwanda yatakayoiwezesha nchi yetu kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

***Ndugu Wahandisi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

4. Ili kutoa picha ya hatua mbalimbali za Mapinduzi ya Viwanda ambazo Dunia imepitia, nitazungumzia kwa kifupi historia ya mapinduzi hayo. Itakumbukwa kuwa kabla ya mapinduzi ya viwanda, ilikuwa ni vigumu sana kwa watu kusafiri kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwani usafiri ulikuwa wa kutumia miguu. Aidha, kusafirisha mazao, vyakula na mizigo mingine au hata kufikisha ujumbe kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ilichukua muda mrefu sana.

   Wakati wa Mapinduzi ya Kwanza ya Viwanda duniani yaliyotokea mwishoni mwa karne ya 18 (mwaka 1765), uvumbuzi wa injini za mvuke (yaani *steam engines*) ulileta mabadiliko makubwa. Uvumbuzi huu ulirahishisha usafiri na kupunguza muda wa kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine. Aidha, Viwanda vya kuendeshwa kwa mikono (yaani *mechanized industries*) vilianza kujengwa na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali uliongezeka kuliko ilivyokuwa kabla ya mapinduzi ya kwanza ya viwanda.

   Mapinduzi ya Pili ya Viwanda duniani yaliyotokea mwishoni mwa karne ya 19 (mwaka 1870) na, yalihusisha uvumbuzi wa nishati ya umeme. Katika mapinduzi haya ya pili ya viwanda, viwanda vya kuendeshwa kwa umeme vilianzishwa, na kukawa na uzalishaji mkubwa wa bidhaa mbalimbali ambazo ziliwaendeleza watu kiuchumi.

Mapinduzi ya Tatu ya Viwanda duniani yalitokea katika kipindi cha pili cha karne ya 20 (mwaka 1969), na yalihusisha uvumbuzi wa teknolojia mbalimbali zikiwemo za kieletroniki, kompyuta na simu. Viwanda vikubwa vilianzishwa na uzalishaji mwingi wa bidhaa viwandani ulikuwa "*automated*", na huduma zinazotumia teknolojia za kisasa kama vile mabenki, matumizi ya mitandao ya kompyuta na simu, na kadhalika zilianzishwa.

Mapinduzi ya Nne ya Viwanda duniani yanahusisha uanzishwaji wa intaneti na teknolojia ambazo zinarahisisha utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Kwa mfano, sasa hivi "*Robots*" zinatumika kufanya kazi ya uzalishaji wa bidhaa viwandani, na kwenye matibabu katika sekta ya afya na kadhalika.

Aidha, teknolojia mpya na matumizi ya TEHAMA katika karne ya 21 yamewezesha kompyuta kutunza takwimu nyingi za aina mbalimbali, kuzichambua takwimu hizo kwa muda mfupi na kutoa mapendekezo kwa matokeo yanayokusudiwa.

Matumizi ya kompyuta zinazofikiria kama watu katika kufanya shughuli mbalimbali nayo yanazidi kuongezeka. Teknolojia hii inajulikana kama "Artificial Intelligence" au "Machine Intelligence". Vilevile katika karne hii tunaona pia "*drones*" zikifanya shughuli mbalimbali, pamoja na kuwepo kwa vyombo vya usafiri kama magari na ndege vinavyojiendesha vyenyewe.

Kwa kifupi, hivi ndivyo ambavyo dunia imepitia katika vipindi mbalimbali vya mapinduzi ya viwanda kuanzia mwishoni mwa karne ya 18 hadi sasa.

*Ndugu Wahandisi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;*

5. lli Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yaweze kuinufaisha nchi yetu, inabidi Wahandisi na Wataalamu wengine nchini kufanya kazi kwa kushirikiana na kwa kutumia ubunifu, weledi na teknolojia za kisasa.

   Napenda kutoa angalizo kuwa, pamoja na fursa zinazoambatana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda, zipo changamoto pia ambazo inabidi zifanyiwe kazi katika maeneo mbalimbali.

   Eneo la kwanza ni katika utoaji wa elimu ya uhandisi. Maandalizi ya Mitaala ya vyuo pamoja na mafunzo ya vitendo inabidi yazingatie mabadiliko haya.

   Eneo la pili ni katika kuboresha mifumo mbalimbali na utoaji wa huduma za uhandisi kwa jamii. Eneo hili linahitaji uwekezaji wa teknolojia, zana na vifaa vipya ambavyo vinaendana na mapinduzi ya nne ya viwanda.

   Eneo la tatu ni katika uboresha utamaduni wa kazi katika sekta ya uhandisi ambapo Wahandisi wanatakiwa kushirikiana kikamilifu na Wataalam wa fani nyingine katika kuleta maendeleo ya kijamii.

   Aidha, ili Taifa letu liweze kujitegemea inabidi Wahandisi wawe watafiti na wabunifu ili kuanzisha mifumo yetu wenyewe ya kitekinolojia ambayo itakuwa endelevu, bila kutegemea nchi zilizoendelea. Hii ni changamoto kubwa lakini kama Taifa, hatuna budi kuitafutia na kuipatia ufumbuzi.

Nimefurahi kusikia kwamba mada zitakazotolewa na wataalam zimegusa sekta mbalimbali zinazochangia ukuaji wa uchumi wa viwanda, kama vile sekta za Maji, Kilimo, Nishati, Miundombinu, TEHAMA na Mazingira.

Rai yangu kwenu ni kuwa kupitia mkutano huu, Wahandisi inabidi mje na mapendekezo ya kisera na kisheria ambayo yataifanya Tanzania kupitia Wahandisi wake iwe tayari kushiriki katika maendeleo yanayotokana na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda kwa viwango vya kimataifa.

***Ndugu Wahandisi, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

6. Baada ya maelezo hayo kuhusu awamu mbalimbali za mapinduzi ya viwanda duniani, sasa napenda kuzungumzia kwa kifupi baadhi ya hatua zinazochukuliwa na Serikali yetu ili kufanikisha Uchumi wa Viwanda hapa nchini.

MRADI WA JULIUS NYERERE HYDROPOWER NA WA UMEME VIJIJINI

Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Nyerere (Julius Nyerere Hydropower) utakaozalisha *Megawatt 2,115 katika Bonde la Mto Rufiji, eneo la Stiegler's Gorge* ili kuwezesha nchi yetu kuwa na umeme wa kutosha kwa ajili ya shughuli za viwanda. Mradi huu pamoja na miradi ya umeme vijijini (maarufu kama miradi ya umeme wa REA) pamoja na kutoa nishati ya umeme kwa matumizi mbalimbali, inalenga pia katika kufanikisha suala zima la kuanzisha na kukuza viwanda katika ngazi zote, hadi katika ngazi ya vijiji. Aidha, lengo la Serikali ni kwamba ifikapo mwaka 2021 jumla ya **vijiji** vyote **12,268** viwe vimeshapata umeme.

Miradi hii ya umeme ni fursa kubwa ya kusaidia kuharakisha maendeleo kwenye sekta mbalimbali zikiwemo sekta za afya, elimu, viwanda, uchukuzi, maji, nishati, maendeleo ya jamii, usalama na nyingine nyingi.

## TANZANIA KUWA NCHI YA UCHUMI WA KIPATO CHA KATI

Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuleta maendeleo na kuinua hali ya maisha kwa watanzania wote. Lengo la Serikali ya Awamu ya Tano wakati inaingia madarakani lilikuwa ni kuifanya Tanzania kuwa Nchi ya Kipato cha Kati kimaendeleo, (yaani *Middle Income Economy)* kufikia mwaka 2025. Hata hivyo, Tanzania imefikia lengo hilo miaka mitano kabla, kwani **Benki ya Dunia mnamo tarehe 1 Julai 2020 imeitangaza Tanzania kuwa katika orodha ya nchi zilizoingia katika uchumi wa kipato cha kati.**

Mafanikio yote haya kwa sehemu kubwa yametokana na juhudi na utashi wa Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wa kusimamia vyema uchumi wa nchi yetu tangu alipoingia madarakani mwaka 2015, na hivyo kuufanya uchumi wa Tanzania kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2019 kukua kwa kiwango cha kuridhisha kati ya **asilimia 6.2** (mwaka 2016) hadi **asilimia 7.0 (mwaka 2019)**. Sababu nyingine kubwa ya mafanikio haya ni utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati iliyoleta ajira kwa watanzania wengi.

## UCHUMI WA VIWANDA

Ili kuongeza pato la Taifa, kuongeza ajira na kuikwamua nchi yetu kutoka katika umasikini, Serikali imeendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kujenga viwanda vipya katika kila mkoa na kufufua vilivyokuwepo. Sote tunashuhudia kufanyika kwa ujenzi wa viwanda kama vya saruji, sukari,

nguo, madawa, madini na kadhalika. Viwanda vinavyojengwa viko katika makundi **manne** tofauti kutegemea ukubwa wa kiwanda husika. Makundi hayo ni: (i) Viwanda Vikubwa (ii) Viwanda vya Kati (iii) Viwanda Vidogo; na (iv) Viwanda Vidogo sana. Katika miaka mitano iliyopita ya Serikali ya Awamu ya Tano, viwanda vipya zaidi ya **8,477** vyenye ukubwa tofauti vimejengwa. Kati ya viwanda hivyo, **vikubwa** ni **201**, **vya kati** ni **460**, **vidogo** ni **3,406** na **vidogo sana** ni **4,410.** Ujenzi wa Viwanda hivi umeongeza ajira za moja kwa moja za viwandani kutoka **ajira 254,786** zilizokuwepo mwaka 2015 hadi kufikia **ajira 482,601** mwaka 2020 ambalo ni ongezeko la **ajira mpya 227,815**.

Aidha, ni dhahiri kuwa kuwepo kwa viwanda hivi kumezalisha pia ajira nyingine nyingi kwa wananchi zisizo za kuajiriwa moja kwa moja viwandani ambazo zimeinua hali zao za kiuchumi na kimaisha.

Wawekezaji wengi zaidi bado wanaendelea kujitokeza kuwekeza katika Sekta ya Viwanda hapa nchini. Uzalishaji viwandani utaendelea kuhitajika na kuongezeka kutokana na kukua kwa soko, hususan kufuatia makubaliano na mikakati mbalimbali ya kikanda ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Uwekezaji wote huo unaoendelea kwa vyovyote vile utahitaji **huduma za Wahandisi kwa kiwango kikubwa.** Hivyo ni muhimu kuwepo kwa utayari (*readiness*) wenu na kuhakikisha kwamba mnajijengea uwezo (*capacity*) unaohitajika ili muweze kuzitumia fursa hizi kikamilifu.

MIRADI MINGINE KATIKA SEKTA MBALIMBALI

Kama mnavyofahamu, Serikali pia inaendelea na ujenzi wa Reli ya Kisasa (*Standard Gauge Railway)* kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora, Dodoma. Ukarabati wa reli zilizopo pia unaendelea kufanyika.

Vilevile, Serikali inaboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo mtandao mkubwa wa barabara nchini kote, madaraja makubwa likiwemo la Kigongo – Busisi, Daraja Jipya la *Selander*, barabara za juu kwenye Makutano ya Ubungo, Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Awamu ya Pili), Miundombinu ya Umeme na Maji, Upanuzi wa Bandari za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara; Ujenzi na Uboreshaji wa Hospitali za Rufaa, Mikoa, Wilaya na Vituo vya Afya, ujenzi na ukarabati wa Vyuo Vikuu, Shule za Sekondari, Shule za Msingi na Shule za Awali.

Katika miaka mitano iliyopita, Serikali ya Awamu ya Tano imesimamia ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege na ufufuaji wa Shirika la Ndege la Taifa. Hadi sasa ndege nane (8) tayari zimeshapokelewa kati ya ndege kumi na moja (11) zilizonunuliwa. Ndege hizo nane zinatoa huduma ndani na nje ya nchi.

## KUANZISHWA KWA WAKALA ZA KUTOA HUDUMA ZA BARABARA NA MAJI VIJIJINI

Serikali imeanzisha Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ili kusaidia kutatua changamoto kubwa ya miundombinu ya barabara za mijini na vijijini. Aidha, Serikali pia imeanzisha Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ili kuboresha na kuharakisha kusambaza huduma za maji vijijini. Rai yangu ni kwamba TARURA na RUWASA wafanye kazi zao kwa weledi na uadilifu mkubwa na kufikia mategemeo na matazamio ya wananchi wengi, hususan wa vijijini ambako

miundombinu ya barabara za uhakika na huduma ya maji safi na salama bado ni changamoto.

UHABA WA WAHANDISI NCHINI

Kama Mwenyekiti wa Bodi alivyoelezea, bado kuna uhaba wa Wahandisi hapa nchini. Idadi ya wahandisi **29,019** waliosajiliwa waliopo ni idadi ndogo kwa mahitaji wa maendeleo ya nchi yetu. Lengo la Serikali ni kuendelea kuongeza na kuimarisha vyuo vyetu vinavyofundisha wahandisi. Serikali imeanza kuchukua hatua za kuongeza majengo katika vyuo, na kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vinavyotoa wahandisi, kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (University of Dar es Salaam – UDSM), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mbeya University of Science and Technology – MUST), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (Dar es Salaam Institute of Technology – DIT), Chuo cha Ufundi Arusha (Arusha Technical College – ATC), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (National Institute of Transport – NIT), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (Sokoine University of Agriculture – SUA), Chuo Kikuu cha Ardhi (Ardhi University – ARU) na Chuo cha Maji (Water Institute – WI).

Vilevile, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kusomesha wataalamu hawa kwa kiwango cha Stashahada na Shahada.

***Ndugu Mwenyekiti wa Bodi na Wahandisi;***

7. Nachukua fursa hii kutoa pongezi kwa Wizara na Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa juhudi zenu za kuendeleza wahandisi wahitimu (ambao kama alivyosema Mwenyekiti wa Bodi idadi yao ni takribani **1,445** kwa

mwaka) kupitia mpango wa *Structured Engineers Apprenticeship Programme (SEAP)*. Nafahamu kwamba mpango huu unahitaji fedha nyingi pamoja na miradi zaidi ya kutolea mafunzo. Serikali inaendelea kuyafanyia kazi masuala haya. Aidha, wakati Serikali na Bodi pamoja na Wadau wengine tukifanyia kazi hatua za kupata vyanzo vingine vya mapato ili kufanikisha zaidi mpango huu, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo haya.

Napenda niipongeze pia Serikali ya Norway kupitia Ubalozi wake hapa nchini kwa kuiunga mkono Serikali kwani wamekuwa wakitoa kiasi kikubwa cha fedha tangu mwaka 2010 kwa ajili ya kuwaendeleza wahandisi wahitimu wanawake. Aidha, naishukuru Benki ya Dunia ambao nao tangu mwaka 2018 wanatoa fedha kupitia mradi wa "Dar es Salaam Urban Transport Improvement Project" kwa ajili ya kuendeleza vijana hawa. Pia, napenda kuishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutoa fedha kupitia mradi wa (*Education and Skills for Productive Jobs* - ESPJ) unaogharamiwa kwa fedha kutoka Benki ya Dunia, kwa ajili ya kuwaendeleza wahandisi wahitimu kuanzia mwaka 2019.

**Ndugu Mwenyekiti wa Bodi pamoja na Ndugu Wahandisi;**

8. Kwa niaba ya Serikali napenda pia kuwapongeza Wahandisi wote hapa nchini kwa ujumla, kwani mmetoa mchango mkubwa katika kufanikisha kazi kubwa ya kuleta maendeleo katika nchi yetu inayofanywa na Serikali hii ya Awamu ya Tano kupitia miradi mingi ya miundombinu, mikubwa na midogo iliyotekelezwa, na inayoendelea kutekelezwa hapa nchini. Watanzania wanapozungumzia kuridhika na hatua kubwa ya

maendeleo ya nchi yetu katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, ni dhahiri kuwa wanazungumzia pia kuridhika kwao na kazi zinazofanywa na ninyi Wahandisi katika kujenga miundombinu wezeshi mbalimbali nchini. Aidha, mnastahili pongezi kwa mchango wenu uliowezesha Tanzania kufikia katika hatua ya uchumi wa kipato cha kati mwaka huu wa 2020. Hongereni sana, na endeleeni kutekeleza wajibu wenu kwa uzalendo, weledi, juhudi na maarifa. Hata hivyo, Bodi iendelee kuwachukulia hatua kali baadhi ya Wahandisi wachache wasiozingatia miiko na maadili ya Taaluma yao ya Uhandisi maana wanaichafua Taaluma ya Uhandisi mbele ya jamii, pamoja na kuisababishia nchi yetu hasara kutokana na vitendo vyao hivyo.

***Ndugu Mwenyekiti wa Bodi, Ndugu Wahandisi;***

9. Kabla sijamaliza hotuba yangu, napenda nirejee Mkutano kama huu uliofanyika mwaka 2018 wakati Bodi yenu inasherehekea miaka 50 ya kuanzishwa kwake, ambapo nilielekeza kuwa niletewe maazimio yenu ya Mkutano ule ambayo yanaainisha changamoto zinazohitaji kuchukuliwa hatua na Serikali. Mnamo mwezi Machi, mwaka 2019, Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi aliwasilisha kwangu Maazimio husika kama nilivyoelekeza. Kwa kifupi, napenda kuwafahamisha kuwa Maazimio yote yaliyowasilishwa kwangu yamefanyiwa tathmini kwa kuzishirikisha Ofisi ya Waziri Mkuu (Sekta ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu); Wizara ya Fedha na Mipango; TAMISEMI; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi); lakini pia niliishirikisha Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa kuelekeza kuwa Bodi ifanye uchambuzi wa kina

kuhusiana na utendaji kazi wa Wahandisi na Makampuni ya Wazalendo nchini na kuandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto zinazosababisha utendaji usioridhisha ili hatimae kuwezesha kuongeza tija na uwezo wa Wahandisi na Makampuni hayo ya Wazalendo kuliko ilivyo sasa.

Kwa nyakati tofauti tayari nimeshapokea mapendekezo ya jinsi ya kutekeleza Maazimio ya Mkutano wa mwaka 2018 kutoka kwa Wizara zote nilizozitaja (pamoja na baadhi ya Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo), lakini pia nimepokea kutoka kwa Bodi ya Usajili wa Wahandisi taarifa niliyoelekeza waifanyie kazi.

Mapendekezo yaliyowasilishwa na Wizara husika pamoja na Bodi ya Usajili wa Wahandisi yamefanyiwa uchambuzi na kubaini kuwa zipo hatua zilizopendekezwa ambazo zinaweza kutekelezwa katika muda mfupi (na baadhi yake zimeanza kutekelezwa), lakini zipo hatua nyingine ambazo utekelezaji wake unahitaji muda wa kati na muda mrefu, hususan zile zinazohitaji maamuzi ya kisera.

Ndugu Mwenyekiti wa Bodi, hivi karibuni nitakuletea taarifa rasmi ya maandishi yenye maelezo ya kina ya jinsi ambavyo Serikali, Bodi yako pamoja na Jumuia ya Wahandisi kwa ujumla tunapaswa kushughulikia maazimio yale ili kufanikisha azma ya kuondoa changamoto zilizopo, na hivyo kuongeza tija na ufanisi zaidi katika sekta hii ya ujenzi.

***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Makatibu Wakuu, Ndugu Mwenyekiti wa Bodi, Wahandisi Wote, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

10. Nimalizie hotuba yangu kwa kuwapongeza tena ninyi wote kwa kushiriki katika maadhimisho haya ya Siku ya Wahandisi, na niwatakie mkutano mwema, na majadiliano yenye tija. Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa Bodi, na kuhakikisha kwamba maazimio yanayofikiwa katika mkutano huu yanafanyiwa kazi, na matokeo yake yanachangia katika kukuza uchumi wa nchi yetu kupitia Sekta ya Viwanda.

Mwisho kabisa, natoa shukrani zangu za dhati kwa Bodi ya Usajili wa Wahandisi, kwa kunipatia **Tuzo** ya kutambua mchango wangu katika Sekta ya Ujenzi, hususan ushiriki wangu katika kuanzisha mpango wa mafunzo (*apprenticeship*) kwa wahandisi wahitimu mnamo mwaka 2003, wakati nilipokuwa Katibu Mkuu katika Wizara ya Ujenzi.

Pamoja na shukrani hizi, nafarijika sana kuona jinsi ambavyo Bodi ya Usajili wa Wahandisi inafanya kazi nzuri ya kutekeleza mpango huu wa mafunzo kwa Wahandisi Wahitimu. Hongereni sana na endeleeni kutekeleza mpango huu ambao una tija kubwa kwa wahandisi wahitimu pamoja na kwa sekta nzima ya ujenzi na Taifa kwa ujumla.

Kama nilivyosema awali, Serikali kwa kushirikiana na Bodi pamoja na wadau wengine, tutaendelea kushirikiana kushughulikia changamoto zilizopo, ili mpango huu uweze kutoa mafunzo kwa Wahandisi wahitimu wengi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Baada ya kusema hayo, ninayo furaha sasa kutamka kwamba **Maadhimisho ya Siku ya Wahandisi kwa Mwaka 2020 nimeyafungua rasmi**.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.**